# KONGAMANO LA 4 LA KIMATAIFA KUHUSU AFYA YA UMMA BARANI AFRIKA

International CPHIA 2024 Conference on Public Health in Africa

**26–29 NOVEMBA 2024 • RABAT, MOROKO**

**KUELEKEA KUJITEGEMEA ILI KUFIKIA HUDUMA YA AFYA KWA WOTE NA USALAMA WA AFYA BARANI AFRIKA**

## Muhtasari wa Wasilisho la Ikisiri za CPHIA 2024

### Kuhusu CPHIA

Kongamano la kila mwaka la Afya ya Umma barani Africa (CPHIA), mradi wa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa barani Afrika (Africa CDC), unatoa mfumo wa kipekee unaoongozwa na Waafrika kwa viongozi na wanasayansi kote barani kushiriki taarifa za maendeleo ya kisayansi, mafunzo tuliyojifunza katika utoaji wa huduma bora za afya, na suluhu bunifu za afya ya umma zenye msingi wa ushahidi ili kushughulikia changamoto za kiafya barani Afrika.

CPHIA 2024 litaandaliwa mjini Rabat, Moroko, kuanzia tarehe 26 hadi 29 Novemba 2024, huku likitarajiwa kushirikisha hadi viongozi 10,000 wa kisiasa, watunga sera za afya, wabunifu na watetezi wa afya, wajasiriamali, wanasayansi watafiti, wataalamu wa afya, wawakilishi wa raia na vijana. Tukio hili, linaloandaliwa kwa pamoja na Africa CDC na Wizara ya Afya na Ulinzi wa Jamii ya Ufalme wa Moroko, litaangazia maendeleo ya Afrika kwenye jukwaa la kimataifa chini ya mada "Kuelekea katika Kujitegemea ili Kufikia Huduma ya Afya kwa Wote na Usalama wa Afya Barani Afrika" na linaangazia nyanja nane za mada.

Hili litakuwa kongamano la nne, la kwanza lilifanyika mwanzoni kwa njia ya mtandao mwaka wa 2021 na kisha la pili na tatu ana kwa ana mnamo mwaka wa 2022 na 2023 huko Kigali, Rwanda, na Lusaka, Zambia, mtawalia. Huku nchi za Afrika zikiharakisha ufanikishaji wa huduma ya afya kwa wote, CPHIA za kila mwaka zinasaidia kubaini jinsi Afrika inaweza kujitegemea zaidi katika utoaji wa huduma bora za afya ili kufikia Afrika yenye afya, ustawi zaidi – kwa bara, na ulimwengu.

### Uwasilishaji wa Ikisiri

Waandaaji wa CPHIA 2024 wanafurahi kukaribisha ikisiri kuhusu nyanja zote za kongamano kutoka kwa washirika wowote husika.

AfricaCDC Centres for Disease Control and Prevention

Limeandaliwa na:

وزارة الصحة والحماية الاجتماعية
Ministère de la Santé et de la Protection Sociale

Waandishi wanapaswa kupakia ikisiri zao kupitia **[jukwaa la wavutini la uwasilishaji wa Ikisiri la Oxford]()**. Iwapo utapata changamoto katika kutumia jukwaa hili, tafadhali wasiliana na CPHIAabstracts@africacdc.org.

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya mwisho ya uwasilishaji** | Tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa ikisiri ni tarehe **23 Septemba 2024 saa 23:59 EAT [(saa 20:59 UTC].** ***Hakuna ikisiri zitakazokubaliwa baada ya tarehe hii.*** |
| **Notisi za kukubaliwa** | Waombaji wataarifiwa kuhusu kukubaliwa kwa maombi yao kufikia tarehe **18 Oktoba 2024.** |
| **Wasilisho** | Ikisiri zilizokubaliwa zitawasilishwa katika kongamano, mnamo tarehe **26 - 29 Novemba 2024.** |

**Tarehe muhimu:**

**Mada:** Ikisiri zitakazokubaliwa zitahusu nyanja na mada ndogo zifuatazo za kongamano:

1. ***Nyanja ya 1:*** Safari ya kujenga usalama wa afya barani Afrika kupitia uwezo wa bara wa kutengeneza bidhaa zote za afya.
   *Mada ndogo:*
   a. Kulinda mahitaji kupitia njia mpya za ununuzi na ugavi (majukwaa yaliyojumuishwa ya ununuzi na ugavi, Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na mageuzi ya ubunifu ya gharama za huduma ya afya na bima ya afya).
   b. Uwekezaji endelevu: Miradi yenye faida na mazingira mazuri kwa biashara endelevu ya kifedha. Kuleta uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni na matumizi ya rasilimali za nchini.
   c. Kujenga mifumo thabiti ya udhibiti: Mamlaka Zilizoimarishwa za Udhibiti wa Kitaifa za Afrika (NRA) na mifumo ya uendeshaji iliyojumuishwa pamoja katika bara zima ikijumuisha jukumu la AMA?
   d. Maendeleo ya hatua kwa hatua ya Utafiti na Maendeleo (R&D) ikiwa ni pamoja na Viambato Amilifu vya Dawa (API): Utafiti, uvumbuzi, na viwango vyote vya majaribio ya kimatibabu.
   e. Kutambua, kujenga na kukuza vipaji muhimu vya kufanya kazi na kuendeleza uwezo wa kutengeneza bidhaa za afya barani Afrika.
   f. Ufadhili na jukumu la sekta binafsi na biashara mpya.
2. ***Nyanja ya 2:*** Kuendeleza hali ya kujitegemea na usalama wa afya kupitia ufadhili bunifu na endelevu wa afya kwa ajili ya huduma ya afya kwa wote barani Afrika.
   *Mada ndogo:*
   a. Kuziba pengo: Kuchunguza na kutathmini mbinu bunifu za ufadhili wa afya kwa ajili ya huduma ya afya kwa wote.
   b. Kudumisha afya kwa wote: Kukuza njia bunifu za ufadhili endelevu wa afya barani Afrika.

    c. Kuhakikisha afya kwa wote: Uhamasishaji wa kimkakati wa rasilimali kwa UHC na usalama wa afya barani Afrika.
    d. Kujenga uaminifu na ustahimilivu: Kukuza utawala na uwajibikaji wa kifedha kwa mifumo ya afya barani Afrika.
    e. Ushirikiano kwa mafanikio: Kuunganisha mikakati ya ufadhili na vipaumbele vya afya ili kubadilisha mifumo ya afya barani Afrika.

3. ***Nyanja ya 3:*** Kuboresha huduma ya afya ya msingi ili kuendeleza huduma ya afya kwa wote barani Afrika.
   *Mada ndogo:*
    a. Kuimarisha usawa wa huduma ya afya ya msingi kupitia ushirikiano wa jamii nzima.
    b. Kuimarisha huduma ya afya ya msingi kupitia teknolojia: Akiliunde, mifumo ya maelezo ya afya na miundo bunifu ya huduma.
    c. Kujenga nguvu kazi ya afya inayofaa kwa kusudi: Kuziba pengo barani Afrika.
    d. Kuimarisha uthabiti wa huduma ya afya ya msingi (PHC) ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza za afya na ustawi.
    e. Kushughulikia viamuzi vya kijamii na kimazingira vya kufanikisha UHC.
    f. Kutekeleza 'Afya katika Sera Zote': Kutambua maono ya tamko la Astana.
    g. Kutumia ushirikiano ili kuimarisha mifumo ya udhibiti wa afya.

4. ***Nyanja ya 4:*** Kuwezesha Afrika yenye afya bora kupitia uvumbuzi wa kidijitali na akiliunde.
   *Mada ndogo:*
    a. Kufanya huduma ya afya ya msingi iwe ya kidijitali: Kutumia mabadiliko ya kidijitali na akiliunde kwa kuboresha utoaji wa huduma.
    b. Afya mahususi na akiliunde: Kuboresha ufanyaji wa maamuzi na utoaji wa huduma.
    c. Kushughulikia tofauti za kiafya kupitia afya ya kidijitali: Jinsia, usawa na ujumuishaji.
    d. Miundo bunifu ya ufadhili kwa suluhu za kidijitali za afya.
    e. Utoaji wa huduma za matibabu kielektroniki na akiliunde (AI): Kupanua ufikiaji na upatikanaji wa huduma za afya.

5. ***Nyanja ya 5:*** Mabadiliko ya hali ya anga na Afya Moja: Kuimarisha usalama wa afya wa Afrika.
   *Mada ndogo:*
    a. Utafiti wa mabadiliko ya hali ya anga na matokeo ya kiafya.
    b. Mifumo ya sera ya Afya Moja na UHC.
    c. Zana za kidijitali za usalama wa afya na utayari wa hali ya anga.
    d. Ushirikishaji wa jamii katika mabadiliko ya hali ya anga na Afya Moja.

6. ***Nyanja ya 6:*** Wanawake na vijana barani Afrika: Kuendeleza afya na uvumbuzi.
   *Mada ndogo:*
    a. Wanawake na vijana kama watumiaji na watoa huduma za afya.
    b. Mbinu ya kudumu ili kupunguza viwango vya vifo vya uzazi na kuboresha mwendelezo wa maisha ya watoto wachanga, watoto na vijana.

c. Kutumia nguvu ya vijana katika Afrika: Kufanya mifumo ya huduma za afya iwe ya kisasa kupitia mifumo ya kidijitali.
d. Athari za kiafya za mabadiliko ya hali ya anga, vurugu na kulazimishwa kuhama kwa wanawake na vijana.
e. Janga la matumizi ya dawa za kulevya linaongezeka kwa kasi barani Afrika – vitisho kwa wanawake na vijana.
f. Kuimarisha huduma ya afya ya msingi ili kuimarisha afya ya mtoto.

7. ***Nyanja ya 7:*** Upeo mpya katika kukabiliana na magonjwa.
   *Mada ndogo:*
   a. Mifumo iliyojumuishwa ya afya ili kukabiliana na magonjwa katika muktadha wa huduma ya afya ya msingi: Changamoto na fursa barani Afrika.
   b. Suluhu na ushirikiano bunifu ili kuzuia na kudhibiti kuongezeka kwa gharama ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza (NCD) na majeraha.
   c. Masomo kutoka kwa uwekezaji na usimamizi wa magonjwa ya kihistoria yenye gharama kubwa (VVU/UKIMWI, Malaria, na TB) ili kuimarisha mikakati ya sasa na kuarifu upeo mpya wa kukabiliana na magonjwa mengine.
   d. Afya ya akili na matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya: Miradi ya afya ya umma iliyofanikiwa kama chunguzi kifani ambazo zinaweza kuigwa kwa kuzingatia muktadha.
   e. Magonjwa ya kitropiki yaliyopuuzwa: Mafunzo yaliyopatikana ili kuharakisha ajenda ya uondoaji.
8. ***Nyanja ya 8:*** Wepesi wa kukabiliana na janga na utayari wa mifumo ya afya kwa uzuiaji bora, ufuatiliaji na ukabilianaji barani Afrika.
   *Mada ndogo:*
   a. Chanjo kama njia bora zaidi ya kuzuia ueneaji wa milipuko: Utengenezaji, kukubalika na wepesi ya matumizi.
   b. Kuendeleza ufuatiliaji wa magonjwa ili kukabiliana na hali za majanga na milipuko.
   c. Jukumu la maabara wakati wa majanga: Kufikia upimaji wa sampuli moja kwa magonjwa mengi yanayotokea ya milipuko.
   d. Ushirikiano wa kimataifa na kieneo kwa usalama wa afya, ikiwa ni pamoja na kukabiliana na janga.
   e. Kushughulikia maelezo potofu na yasiyo ya kweli katika kukabiliana na janga.
   f. Uvumbuzi kwa ufuatiliaji wa sekta mbalimbali na kukabiliana na magonjwa yanayojitokeza na yanayojitokeza tena.
   g. Taasisi za kitaifa na za kieneo za afya ya umma.

**Ustahiki wa Ikisiri na Waandishi:** Ikisiri zilizo na kazi asili katika nyanja zilizo hapo juu ndizo tu zitakazokubaliwa kwenye kongamano. Mwandishi wa msingi lazima awe ameshiriki katika shughuli zilizotajwa kwenye ikisiri na kupata vibali muhimu vya serikali ambapo data nyeti inatumiwa kwenye ripoti, pamoja na hati zozote zinazofaa mahitaji ya uadilifu.

Ingawa mtu anaweza kutuma zaidi ya ikisiri moja, tutakubali tu ikisiri moja kwa kila mtu (mwandishi wa msingi). Utafiti unapaswa kuwa umefanywa katika kipindi cha mwaka 2021-2024 ili kuhakikisha unafaa kwenye mazingira ya sasa ya Afrika. Ikisiri ambazo ziliwasilishwa mahali pengine hapo awali zitazingatiwa kwa hiari ya jopo la uamuzi, lakini kipaumbele kitatolewa kwa ikisiri ambazo bado hazijawasilishwa kwenye kongamano lingine lolote la kisayansi. Waandishi wanapaswa kusisitiza jinsi kazi iliyofanywa ilitumiwa kuleta athari inayofaa kwenye mazingira ya huduma ya afya na/au jinsi utafiti utakavyobadilisha huduma za afya ya umma katika siku zijazo.

**Ukinzani wa Maslahi:** Waandishi wa ikisiri zilizokubalika watalazimika kutuma fomu ya ufichuzi wa ukinzani wa maslahi ambayo itaambatishwa kwenye barua ya kukubali ikisari.

**Ufadhili wa Ikisiri:** Huenda kukawa na ufadhili kiasi wa masomo unaopatikana ili kugharamia usajili, usafiri na malazi kwa wawasilishaji wa mapema wa ikisiri za taaluma. Lazima uwe na umri wa miaka 40 au chini, uwe mwanafunzi wa Uzamili/PhD au umepata MD, Uzamili au PhD katika miaka 5 iliyopita ili ustahiki. Ikiwa ungependa kuomba ufadhili wa masomo, utaombwa wakati wa mchakato wa kutuma ikisiri, uteue kisanduku ikiwa ungependa kuzingatiwa kupata usaidizi huu.

Ili kuomba msaada, unahitajika kujumuisha taarifa pamoja na ikisiri yako. Hata hivyo, tafadhali kumbuka kuwa kuashiria ungependa msaada *sio hakikisho* kwamba utateuliwa kupata ufadhili. Hakuna ufadhili utakaotolewa kwa wanaotuma ikisiri ambao ikisiri zao hazijachaguliwa kwa mawasilisho ya kuzungumza au ya mabango. Wanaotuma ombi wataarifiwa ikiwa wamepata ufadhili wowote pamoja na taarifa ya kukubaliwa au kukataliwa kwa ikisiri zao.

## Muundo wa Ikisiri

**Idadi ya maneno**: Ikisiri haipaswi kuzidi **maneno 300** (ambayo yanajumuisha mada ndogo lakini hayajumuishi mada, maneno muhimu, orodha ya waandishi na anwani zao).

**Waandishi:** Waandishi wanapaswa kuorodheshwa kama ifuatavyo:
- Mwandishi wa kwanza: Andika jina la kwanza, herufi ya kwanza ya jina la kati (ikiwa lipo), na jina la mwisho (k.m., Henry M. Kuku).
- **Waandishi wenza**: Orodhesha kila mwandishi mwenza kulingana na mchango wake kwa kuandika herufi za kwanza za majina yake ya kwanza na ya kati, zikifuatiwa na jina kamili la mwisho (k.m., J.N. Toto, C.H. Kwakweri).
- Andika uhusiano wa kimashirika kati ya mwandishi wa kwanza na waandishi wenza wote.
- Onyesha mwandishi husika kwa kinyota* na uweke anwani ya barua pepe na nambari yake ya simu pamoja na anwani zake mbadala.

**Maneno muhimu**: Tafadhali jumuisha maneno 4 – 6 muhimu

**Mada**: Mada inapaswa kuwa ya kuelimisha lakini iwe kifupi bila mada ndogo au vifupisho/akronimu na inapaswa kuangazia - mada/utafiti unahusu ***nini***, ulifanyika ***wapi*** na ulifanywa ***lini*** (k.m., Kundi la visa vya COVID-19 katika wilaya ya Keke, Agosti 2021). Andika mada katika muundo wa sentensi na uandike tu herufi ya kwanza ya nomino za kipekee na majina ya kisayansi kwa herufi kubwa pale inapofaa (k.m., Plasmodium *falciparum*).

**CHAGUO LA 1: Kwa ikisiri za kisayansi**

**Utangulizi/Usuli**: Shughulikia utangulizi wa kisayansi, mantiki ya utafiti, pamoja na umuhimu wa mada kwenye afya ya umma. Kwa sababu ya uanuai unaotarajiwa wa wakaguzi na wahudhuriaji wa kongamano, usichukulie kuwa kila mtu atafahamu mada yako. Fafanua kwa nini utafiti wako ni muhimu na maswali ambayo utafiti utajibu. Utangulizi uliobainishwa vizuri huvutia hadhira na unapaswa kujumuisha:

- Maelezo mafupi ya mada na umuhimu wake kwa afya ya umma
- Malengo ya utafiti
- Maswali ya utafiti au nadharia tete ya utafiti ikiwa inatumika

**Mbinu**: Eleza mbinu zilizotumika kwenye utafiti. Hoja muhimu zitakazojumuishwa ni pamoja na:

- Muundo wa utafiti
- Mazingira ya utafiti
- Kundi la watu waliofanyiwa utafiti
- Vigezo vya ustahiki na ufafanuzi wa vielelezo, ikiwa vipo
- Ukubwa wa sampuli na mbinu za sampuli
- Udhibiti na uchanganuzi wa data

**Matokeo**: Wasilisha matokeo muhimu (mazuri na mabaya) ya utafiti ambayo yanahusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti. Sehemu hii **haipaswi** kujumuisha majadiliano ya matokeo. Andika nambari kamili na asilimia/ikisami, viwango na uwiano wake panapohitajika. Tafadhali kumbuka, kwa kuwa ikisiri ni hati inayojitegemea na inayoweza kudondolewa, sehemu ya matokeo inapaswa kujumuisha data.

Haipaswi kujumuisha kauli kama vile “Data itajadiliwa.” Ikiwa kazi kubwa bado haijakamilika kabla ya kutuma kwenye kongamano, tafadhali onyesha kuwa matokeo hayajakamilika.

**Hitimisho**: Andika maelezo mafupi iwezekanavyo. Usitaje tena data iliyojumuishwa kwenye matokeo. Sehemu hii inaweza kujumuisha:

- Ufasiri wa matokeo muhimu na athari zake kwa huduma ya afya ya umma
- Hatua za afya ya umma ambazo zimependekezwa na/au zimetekelezwa kutokana na matokeo ya utafiti

- Taarifa za kuhitimisha kama vile matokeo yatajadiliwa hazikubaliki

**CHAGUO LA 2: Kwa ikisiri za sera na mipango**

Ikiwa una mambo uliyojifunza kupitia mipango, miradi au utekelezaji wa sera na mikakati, unaweza kuwasilisha ikisiri inayofuata muundo huu mbadala:

- **Usuli:** Fanya muhtasari wa madhumuni, wigo wa kazi na malengo ya mpango, mradi, sera au mkakati.
- **Maelezo:** Eleza kipindi cha utekelezaji, mazingira na eneo, muundo, idadi ya watu muhimu (ikiwa wapo) na shughuli na hatua zilizochukuliwa.
- **Mambo Uliyojifunza:** Wasilisha kwa kina matokeo ya mpango, mradi, sera, au mkakati. Wasilisha uchambuzi au tathmini ya mambo muhimu uliyojifunza na mbinu bora.
- **Hitimisho/hatua zinazofuata:** Eleza umuhimu wa matokeo ya mpango, mradi, au sera.

***Kumbuka:*** Huwezi kufanya mabadiliko kwenye ikisiri ya mwisho baada ya kuituma. Hata hivyo, katika tukio ambalo ikisiri yako imechaguliwa kwa ajili ya uwasilishaji na imefanyiwa mabadiliko makubwa baada ya kukubalika, mabadiliko hayo yanapaswa kuangaziwa katika wasilisho au bango la ikisiri.

## Vigezo vya Utathmini

Kila ikisiri itatathminiwa na wakaguzi huru kwa kutumia vigezo vifuatavyo:

- Utangulizi na mantiki ya utafiti
- Ufaaji wa mbinu au maelezo
- Uwasilishaji wa matokeo
- Hitimisho na ufasiri wa matokeo
- Umuhimu katika afya ya umma
- Udhahiri wa jumla wa ikisiri
- Mambo mapya kwenye utafiti
- Ufaaji kwenye nyanja/mada ya kongamano

## Maamuzi na Hatua Zinazofuata

**Uchapishaji kwenye Kitabu rasmi cha Ikisiri cha 2024:** Ikisiri zote zilizokubalika zitachapishwa katika Kitabu rasmi cha Ikisiri cha CPHIA 2024.

**Uchapishaji katika Jarida la Afya ya Umma Afrika:** Idadi fulani ya waandishi wa ikisiri zinazokubalika pia watapewa msaada kutoka kwa Africa CDC katika kuandika hati zao ili kuchapishwa katika Jarida la Afya ya Umma barani Afrika la Africa CDC.

**Mawasilisho ya moja kwa moja na ukumbi wa mabango:** Mkutano wa CPHIA 2024 utakuwa wa ana kwa ana. Watu wote wanaotuma ikisiri, iwe wamechaguliwa kwa

mawasilisho ya kuzungumza au ya mabango, wanatarajiwa kuwa na uwezo wa kuhudhuria kongamano katika mji wa Rabat, Moroko.

**Kwa maelezo zaidi kuhusu CPHIA 2024, tembelea www.cphia2024.com. Kwa maswali kuhusu mpango wa ikisiri, tafadhali tuma barua pepe kwa CPHIAabstracts@africacdc.org.**